
# KINACHOJULIKANA KAMA

# UPENDO

## MTAZAMO WA VIJANA




# Shukrani


Kitabu hiki cha katuni kimeandikwa kwa pamoja na vijana kutoka TAMASHA nchini Tanzania na programu ya Lewisham Young Mayor na Young Advisors nchini Uingereza, ikijumuisha baadhi ya watu wafuatao: Dedi Mwita, Lilian Mmbaga, Scola Sumari, Sadam Ahmed, Noel Henry, May Zullu, Mkelemi Abdulrahman, and Elizabeth Emanuel. Kwa msaada wa Churchill Shakim, Katy Brown na Clare Coultas.

Kitabu cha katuni kinatokana na utafiti uliofanywa na Dkt. Clare Coultas kutoka King's College London na kufadhiliwa kwa Ruzuku ya Kuongeza Kasi ya Matokeo ya ESRC (ES/T501931/1).

Kazi zote za sanaa zilifanywa na Victor Ndula.



KATIKA MTAA MMOJA NCHINI TANZANIA, BHOKE ANAMWELEZA RAFIKI YAKE ZAWADI KUHUSU WAZAZI WAKE WANAVYOTAKA AACHE CHUO NA KUOLEWA NA MWANAMUME HUKO KIJIJINI MWAO. WAKIPITA MBELE YA BANGO LINALOELEZEA KUHUSU AFYA YA NGONO, MAJADILIANO YANAGEUKA KUWA TATIZO LA 'MACHAGUO' ...
CHAGUA MPENZI MMOJA, CHAGUA UPENDO, PATA MAISHA ZAIDI
TRUTHLIFE NGO
SIJUI LA KUFANYA. SITAKI KUACHA CHUO NA JIJI LAKINI PIA SITAKI KUWAVUNJA MOYO WAZAZI WANGU.
MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI HUFANYA MAMBO YAONEKANE KUWA RAHISI SANA LAKINI KUCHAGUA NI JAMBO LA UTATA SANA.
NA WAKATI MWINGINE HAIONEKANI KAMA TUNAWEZA KUFANYA UAMUZI.
SISI HATUNA CHA KUCHAGUA, HAYO MAMBO, NI KWA AJILI YA WATU WANAOISHI MAISHA MAZURI BARANI ULAYA NA AMERIKA.



NAKUBALIANA NA WEWE DADA, ELIMU HII YA MAHUSIANO MAZURI NI MANENO MATUPU. NI SAWA NA KUMPA MTU JEMBE BILA MAHALI PA KULIMA. JEMBE HILO LITAKUWA NA MANUFAA GANI?
CHIPS MAYAI
LAKINI HIYO HAIMAANISHI KWAMBA TUNAPASWA KUKATA TAMAA.
HAPANA, HATUZUNGUMZI KUHUSU KUKATA TAMAA, ILA TUNAAMBIWA TUCHAGUE MAISHA BORA LAKINI UKWELI WA MAISHA YETU UNAMAANISHA KWAMBA HATUNA CHA KUCHAGUA HAYO.
Arsenal


WAKATI WOWOTE UKIWA NA SHIDA SIMAMA KARIBU NAMI... NJOO, NJOO, SIMAMA HAPA...
AISEE, MUZIKI HUO UNATOKA WAPI?
NI KAMA UNANIITA, HEBU TWENDE TUKAONE. JINA LANGU NI MASHAKA.
HAYA MASHAKA, VIPI KUHUSU CHIPS MAYAI YAKO?
Arsenal


WAAH!
NI NINI KINACHOENDELEA?
TNG


KUNDI LA WATANZANIA LINAONEKANA NJE YA KITUO CHA VIJANA CHA TNG AMBAPO KUNDI LA VIJANA WATATU WAMESIMAMA.
ATI NINI?!! UMETOKA WAPI?
SISI NI... TUKO WAPI?
BHOKE, UNAZUNGUMZA KIINGEREZA, KAMA MWINGEREZA, KWA LAFUDHI NA KILA KITU!
KULIKUWA NA MWEKO WA NURU AMBAO KARIBU UTUPOFUSHE KISHA GHAFLA UKAJA! SALALAA!
HILI NI JAMBO LA KUSHANGAZA. SEKUNDE MOJA TU ILIYOPITA TULIKUWA NCHINI TANZANIA.



AJABU! UKO NCHINI UINGEREZA SASA! KWA UHAKIKA KABISA UKO KATIKA KITUO CHA VIJANA CHA TNG HAPA LEWISHAM, LONDON.
UINGEREZA! KWELI?
KULIKUWA NA KITU KAMA LANGO KUBWA.
HEBU NIANGALIE [KWENYE SIMU YAKE] NI WAPI ULIPO UBALOZI WA TANZANIA, LABDA WANAWEZA KUWASAIDIA... NDIYO UPO KARIBU NA MTAA WA BOND, TUNAWEZA KUWAPELEKA HUKO. JINA LANGU NI AYLA.
MEI
BHOKE
Tanzania High Commission London
Bond Street
Embassy
London Marriott Hotel Grosvenor Square
Claridge's
Brook Street
Brook's Mews
Grosvenor St
Davies St
Welbeck St
A5204
Bourdon St
OLLIE
ZAWADI
MASHAKA


TUNAWEZA KUSAFIRI KWA BASI, KISHA KWA BOTI NA KUKUONYESHA BAADHI YA MAENEO YA JIJI LA LONDON TUKIWA NJIANI! NILILIPWA JANA KWA HIVYO NAWEZA KULIPIA SAFARI YENU KWA KUTUMIA KADI YANGU.
KITU GANI HIKI KINATOKEA! SIWEZI KUACHA HII FURSA. LABDA NI NAFASI YANGU YA KUTOROKA ILI NISIOLEWE NA YULE MWANAMUME WA KIJIJINI! LABDA NINAWEZA KUKUTANA NA MWANAUME MZURI WA KIINGEREZA AMBAYE ATANIOKOA NA KUNITUNZA KWA SIKU ZANGU ZOTE!
Hard Rock CAFE
Hard Rock CAFE
HAYA JAMANI NIMELIPA!
UNALAZIMISHWA KUOLEWA? HIYO INASIKITISHA SANA! NILIWAHI KUTAZAMA KIPINDI CHA TELEVISHENI KUHUSU NDOA ZA UTOTONI BARANI AFRIKA. LABDA TUNAWEZA KUWASHIRIKISHA POLISI WA HAPA AU SERIKALI YETU... HAKIKA KUNA JAMBO TUNALOWEZA KUFANYA?!



WAZAZI WANGU HAWANILAZIMISHI, NI KWAMBA TU SISI NI MASKINI. NIKIOLEWA NA MWANAMUME HUYU ATAWAPA PESA AMBAZO ZITAMLIPIA MDOGO WANGU ADA YA SHULE.
FAMILIA YANGU PIA WANATAKA NIOLEWE LAKINI KUISHI KWAO HAKUTEGEMEI JAMBO HILO. SAMAHANI BHOKE, HIYO YAKO NI ZAIDI.
NILIDHANI WATU WANAOISHI BARANI ULAYA WAPO HURU KUISHI NA KUWA NA MAHUSIANO WAPENDAVYO!
WENGI WETU TUNA WAZAZI KUTOKA NCHI NA TAMADUNI NYINGINE AMBAZO ZINA MAONI YAO KUHUSU JINSI TUNAVYOPASWA KUISHI MAISHA YETU.
LAKINI PIA HATA FAMILIA ZA WAINGEREZA WEUPE ZINAWEZA KUWASHINIKIZA WATOTO WAO NAMNA YA KUFANYA AU KUJARIBU KUTUZUIA KUWA NA AINA FULANI ZA MAHUSIANO.


MIMI PIA NAWEZA KUHISI JINSI MTU ANAVYOWEZA KUSHINDA NA NJAA NA HUKU AKIWAJIBIKWA KWA AJILI YA NDUGUZE WADOGO. HAPA WATOTO WANAWEZA KWENDA SHULE BILA ADA LAKINI IWAPO MWALIMU AU MTU FULANI ANAHISI KWAMBA HATUWATUNZI VIZURI BASI SERIKALI INAWEZA KUWACHUKUA.
KWA HIYO KUNA WATU MASKINI HAPA PIA?
NDIYO, NI WENGI. LONDON NI AINA YA JIJI AMBAPO UNAWEZA KUWA NA VYUMBA VIKUBWA VYA GHOROFA AMBAPO FAMILIA NZIMA WAMEJAZANA KATIKA CHUMBA KIMOJA AU VIWILI.
... NA UPANDE MWINGINE WA BARABARA UNAWEZA KUONA MATAJIRI WANAOISHI KATIKA MAJUMBA MAKUBWA.
NA PIA KUNA WATU WENGI AMBAO WAPO KATIKATI, WANAWEZA KUISHI KATIKA NYUMBA NZURI LAKINI BADO WANAHANGAIKA KWA SABABU MAISHA JIJINI LONDON NI GHALI.
NINATUMAINI KULIPIA SAFARI YETU HAKUTAKUWA NA TATIZO KWAKO, MEI?
ASANTE KWA KUULIZA ZAWADI, LAKINI NITATAFUTA SULUHISHO. HIKI NDICHO KITUO CHETU, HEBU TUSHUKE.



PIA TUNAONA WATU WENGI ZAIDI WAKILAZIMIKA KUISHI MITAANI NA MARA TU UKIPOTEZA NYUMBA YAKO INAKUWA VIGUMU KUIPATA TENA, KWA SABABU HUWEZI KUPATA KAZI AU HATA KUFUNGUA AKAUNTI YA BENKI BILA KUWA NA ANWANI YA MAKAZI.
UMASKINI UNAWEZA KUONEKANA TOFAUTI HAPA, LAKINI BADO NI MAPAMBANO YA KUENDELEA KUISHI.
GREENWICH MARKET
sophia & matt


ULAYA TUNAYOIONA KWENYE TELEVISHENI HAIKO HIVI. TUNAONA NGUO NA VITU VYA BEI GHALI PEKEE NA NDOTO ZINAZOTIMIA...
HAHA HAPANA! MAISHA YA KWELI HAYAKO HIVYO HATA KIDOGO.
EENWICH
ARKET
LAKINI NINAELEWA NI KWA NINI UNAFIKIRIA HIVYO. NADHANI FILAMU, VIDEO ZA MUZIKI NA VIPINDI VYA TELEVISHENI VINAWEZA KUWASILISHA MAMBO KWA TOFAUTI KAMA VILE KUFANYA IONEKANE KAMA MAISHA NI MAZURI HAPA NA MABAYA KWINGINEKO, WAKATI MAISHA NI TOFAUTI TU, YENYE MAMBO MAZURI NA MABAYA.
LAKINI ANGALAU UNAWEZA KUWA NA UPENDO WA KWELI HAPA. KULE KWETU TANZANIA KILA MTU AANAPAMBANA KIVYAKE. HAKUNA UAMINIFU, HAKUNA MAWASILIANO... MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI HUZUNGUMZA KUHUSU JINSI TUNACHOHITAJI KUFANYA NI KUCHAGUA KUWA NA UHUSIANO MZURI AU KUCHAGUA UPENDO LAKINI SIJUI MTU YEYOTE AMBAYE AMEWEZA KUFANYA HIVYO.



ZAWADI KWA KWELI UNAZUNGUMZA KAMA RAFIKI YETU AMBAYE HIVI KARIBUNI ALIACHANA NA MPENZI WAKE. ALIMDANGANYA SANA NA KWA KWELI ALIMVURUGA NA SASA ANASEMA HAAMINI KWAMBA KUNA UPENDO. LAKINI NADHANI HUO NI MOYO ULIOVUNJIKA UNAOZUNGUMZA. NI VIGUMU KUFIKIRIA KWAMBA MAMBO MAZURI YANAWEZEKANA TUNAPOUMIA AU KUHISI KAMA TUMEZUNGUKWA NA UBAYA.
LAKINI PIA MAHUSIANO MAZURI HAYATOKEI MARA MOJA KAMA VILE SINEMA ZA HOLLYWOOD NA MAGAZETI ZINAVYOKUFANYA UAMINI. KUFANIKIWA KWA MAHUSIANO KUNACHUKUA MUDA, JITIHADA NA UVUMILIVU KUTOKA KWA WOTE WAWILI.
Greenwich Pier
Westminster Embankment
NADHANI TUNAPAMBANA NA MATARAJIO KATIKA MAHUSIANO YETU NCHINI TANZANIA. FAMILIA ZETU NA MARAFIKI WA KIKE WOTE WANATARAJIA SISI WANAUME TUTIMIZE MAHITAJI YAO NA INATULAZIMU KUJITAHIDI ILI KUFANYA HIVYO, LAKINI MAISHA NI MAGUMU NA MARA NYINGI HATUWEZI...
NA WANAUME WANAONA AFADHALI WASEME UWONGO KUHUSU JAMBO HILI KULIKO KUWA NA MAZUNGUMZO YA WAZI NA WAPENZI WAO.
LAKINI TUNAPOSHINDWA KUTIMIZA MAHITAJI YA WAPENZI WETU WA KIKE, WANAFIKIRI KWAMBA HATUJALI NA BADO FAMILIA ZETU ZINATAKA TUOANE JAPO HATUNA PESA. KWA NINI TUONGELEE MAPUNGUFU YETU?


SIDHANI KAMA TUNAVYOPATA SHIDA KUZUNGUMZIA MATARAJIO TOFAUTI KUNATUFANYA TUONEKANE WA TOFAUTI. KUWASILIANA NI JAMBO GUMU. PIA NI LA KITAMADUNI. FAMILIA YANGU, KWA MFANO, NI YA KIDINI NA SINA UHAKIKA KAMA HAYA NDIYO MAISHA NINAYOTAKA. BADO SIJAPATA NJIA YA KUZUNGUMZA NAO KUHUSU JAMBO HILO.
PIA NADHANI NI VIGUMU KUSIMAMIA MAMBO YA PESA KATIKA MAHUSIANO MENGI. MARA NYINGI PESA HUAMBATANA NA HISIA ZA KUJITHAMINI. WAKATI HUNA CHOCHOTE UNAWEZA KUHISI KWAMBA HUNA THAMANI NA NI VIGUMU SANA KUZUNGUMZA NA WENGINE KUHUSU HALI HIYO KAMA UNAJIHISI HIVYO.
NADHANI KILE AMBACHO WENGI WETU WANATAKA MAISHANI NI KUJISIKIA KAMA TUNA THAMANI NA UNASEMA KWELI MEI, MARA NYINGI INAHUSISHWA NA PESA. TUNAPOKUWA NA MAVAZI MAZURI NA VITU VIZURI KILA MTU ANATAKA KUWA RAFIKI YETU.
WASICHANA WANAHUKUMIWA VIKALI HAPA PIA. MVULANA ANAPOKUWA NA WAPENZI WENGI ANAONEKANA KUWA MJANJA, NA ANAPENDWA ILA KWA MSICHANA IKITOKEA HIVYO BASI ATAITWA MAJINA YOTE MABAYA NA KUEPUKWA NA WENGI.
SIKU ZOTE NIMEKUWA NIKIFIKIRIA KWAMBA THAMANI YANGU INGETAMBULIWA NIKIOLEWA.
MAMBO HALISI YA KIJINSIA YANAWEZA KUBADILIKA KULINGANA NA MAHALI ULIPO ULIMWENGUNI, LAKINI BADO YAPO KILA MAHALI. WANAWAKE HAPA WANALIPWA KIASI KIDOGO KULIKO WANAUME, TUNANYANYASWA KINGONO NA KUNA WACHACHE KATI YETU WALIO NA NYADHIFA ZA MAMLAKA. HALI NI MBAYA ZAIDI KWA WANAWAKE WASIO NA ASILI YA KIZUNGU.
NADHANI HOLLYWOOD NA DISNEY WAMETUVURUGA SANA KWA KUFANYA MAMBO YAONEKANE NI 'RAHA MUSTAREHE SIKU ZOTE' NA HIKI KITU KINACHOITWA UPENDO KINAFANYA MAISHA KUWA NA RAHA TUPU.


WALIANZA SAFARI YAO YA BOTI KWENYE MTO THAMES.
TOWER HILL
Canary Wharf Ferry
CANARY WHARF
Woolwich Ferry
Bankside Pier
Festival Pier
Waterloo Millennium Pier
Millbank Millennium Pier
PIMLICO
Canary Wharf Pier
ISLE OF DOGS
QEII Pier (Millennium Pier)
RIVER THAMES
Masthouse Terrace Pier
Barrier Gardens Pier
Woolwich Pier
NDIYO, KAMA ALIVYOSEMA MEI HAPO AWALI MAISHA HALISI HAYAWEZI KUGAWANYWA KWA URAHISI KUWA 'MAZURI' NA 'MABAYA'. MAISHA NI MVURUGO MMOJA MKUBWA WA MEMA NA MABAYA NA KATIKATI YA HAYO. KWANGU MIMI, NADHANI UHUSIANO MZURI NI ULE AMBAO UNA NAFASI YA KUKUA, KWA SABABU KINACHOMFURAHISHA KILA MTU KINAWEZA PIA KUBADILIKA BAADA YA MUDA NA JITIHADA ZINAHITAJIKA ILI MABADILIKO KAMA HAYO YAWEZE KUTOKEA KWA KILA MTU.
KWANGU MIMI NI KUELEWA DHAMIRA YAKO MAISHANI. BILA SHAKA, MIMI, KAMA ZAWADI, NATARAJIA KUPATA MTU AMBAYE ATANIJALI, LAKINI PIA NINAAMINI KWAMBA HILI LINAANZA NA MIMI. LAZIMA NIWE NA UHUSIANO MZURI KWA KUJIPENDA MIMI MWENYEWE KABLA YA KUWA NA UHUSIANO MZURI NA MTU MWINGINE. NIMEPATA DHAMIRA HIYO KATIKA MAFUNZO YA KUWA MEKANIKA NA PIA NINAPATA NGUVU KUTOKA KWA MARAFIKI ZANGU.
NI VIGUMU SANA KUPATA KAZI NCHINI TANZANIA NA MAISHA YANAWEZA KUFANYA MTU AHISI KUTOKUWA SALAMA, LAKINI SISI PIA TUNAPATA NGUVU KATIKA URAFIKI WETU. TUNASEMA 'TUKO PAMOJA' NA 'TUNAINUKA MAISHANI'
MAISHA KWA UJUMLA YANAONEKANA KUTOKUWA SALAMA HIVI SASA, KWA SABABU YA MABADILIKO YA TABIA-NCHI NA UKATILI UNAOONGEZEKA ULIMWENGUNI KOTE. NI VIGUMU KUENDELEA KUWA NA IMANI KUKIWA NA SINTOFAHAMU.
LAKINI NI WAKATI HUU AMBAPO IMANI NI JAMBO MUHIMU. HATA IKIWA HUNA DINI.


HII NDIYO SABABU TUNAFADHAISHWA SANA WAKATI MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI YANAPOZUNGUMZA KUHUSU KUCHAGUA. NINAPENDA CHUO LAKINI NINA SHAKA IWAPO NINAWEZA KUISHI BILA PESA ILI FAMILIA YANGU IPATE MLO, SEMBUSE KULIPA ADA YA SHULE. UTACHAGUA NINI HAPA?
NAFIKIRI CHOCHOTE KITAKACHOTOKEA, TAFADHALI BHOKE, USIONE KAMA KUPOTEZA FURSA KABISA MAISHANI. NAJUA MWANAMKE AMBAYE ALILAZIMIKA KUACHA SHULE WAKATI ALIPOPATA UJAUZITO, LAKINI SASA KWA KUWA WATOTO WAKE WAMEKUA, AMERUDI SHULENI!
KAMA MAMA AISHA, BHOKE AMEKUWA NA MAISHA MAGUMU SANA LAKINI HAJAWAHI KUKATA TAMAA. SIKU ZOTE ANAIFANYIA KAZI JAMII YAKE NA ANAWEKA AKIBA YA PESA ILI AWEZE KUSOMA KOZI ZA MTANDAONI ILI AJIENDELEZE YEYE NA FAMILIA YAKE.
NIMEFURAHI SANA KWAMBA TUMEKUTANA NANYI NYOTE. INAWEZA KUONEKANA KUWA MAMBO NI MABAYA, LAKINI KUJUA KWAMBA WATU WANAPAMBANA NA MAHUSIANO YAO, NIJIONE KUWA SIPO PEKE YANGU.
PIA NINAHISI KUWA NA NGUVU ZAIDI... KANA KWAMBA MAPAMBANO NI KITU KINACHOTUUNGANISHA.


KUNDI LINASHUKA KWENYE WESTMINSTER PIER.
NAAMINI SIKU MOJA TUTAWEZA KUWATEMBELEA NINYI NYOTE NCHINI TANZANIA. BAADA YA KUZUNGUMZA NANYI NAJUA HAITAKUWA KAMA INAVYOONYESHWA KWENYE TELEVISHENI. KAMA WEWE ZAWADI NADHANI MAPAMBANO YETU YANAWEZA KUUNGANISHWA ZAIDI KULIKO TULIVYOFIKIRIA.
WAKATI WOWOTE UKIWA NA SHIDA SIMAMA KARIBU NAMI... NJOO, NJOO
AMA HAPA...
AISEE, KILA MTU... SHHH! SIKILIZENI! NI WIMBO HUO TENA. HIVI NDIVYO TULIVYOKUJA HAPA KUTOKA TANZANIA!
UNAMAANISHA LANGO KUBWA?
NDIYO! NJOO, HEBU TUANGALIE. OLLIE, UMESEMA KWAMBA UNATAKA KUJA TANZANIA, ULIKUWA NA UHAKIKA?


NDIYO! HEBU TUFANYE HIVI!
TANZANIA, TUKO NJIANI!!



WOTE WANASHIKANA MIKONO WANAPOPITIA KWENYE LANGO KUBWA, WAKIWA TAYARI KUANZA SAFARI YAO NCHINI TANZANIA
WAKATI WOWOTE UKIWA NA SHIDA SIMAMA KARIBU NAMI... NJOO, NJOO, SIMAMA HAPA...
WOOA!
TAZAMA UKURASA UNAOFUATA KWA MASWALI AMBAYO UNAWEZA KUTUMIA ILI KUKUSAIDIA KATIKA MAJADILIANO YAKO KUHUSU MAMBO AMBAYO YAMEONGELEWA KATIKA SIMULIZI HII NA PIA KILE KINACHOWEZA KUTOKEA BAADAYE!

# Maswali ya Kujadili/Kufikiri

1. Vijana katika katuni waliona ujumbe kuhusu jinsi tunavyopaswa kuchagua upendo, kuchagua kuwa na mahusiano 'mazuri' na kuchagua maisha 'mazuri'.
   - Ujumbe huu huwafanya vijana wajisikie vipi?
   - Je, vijana wanahisi kwamba wana uhuru wa kuchagua?

2. Baadhi ya vijana hao wanatoka Tanzania na wengine wanatoka London (Uingereza).
   - Vijana Watanzania wanaamini nini kuhusu maisha barani Ulaya? Imani hizi ni sahihi au si sahihi kwa kiasi gani?
   - Vijana wa London wanaamini nini kuhusu maisha barani Afrika? Imani hizi ni sahihi au si sahihi kwa kiasi gani?
   - Imani potofu au imani zisizo sahihi zinaweza kuwa na athari gani? (k.m. zinaweza kuathiri vipi jinsi vijana wanavyofikiria kuhusu wao wenyewe, wengine na ulimwengu kwa ujumla?)
   - Unafikiri vijana wa London watajifunza nini watakapokwenda Tanzania?

3. Hadithi imeonyesha kwamba mapambano ya uhusiano huunganisha watu kutoka maeneo tofauti, hata ikiwa mapambano haya yanaweza kuonekana au kuhisi kuwa tofauti kidogo.
   - Baadhi ya migogoro ya kawaida ya uhusiano ni ipi?
   - Tunawezaje kusaidiana katika mapambano haya? (k.m. Tunaweza kuzungumzia vipi tena mahusiano katika kampeni za elimu ya ngono na afya ikiwa hatuzingatii 'uchaguzi' na 'kitu chema'?)



# KINACHOJULIKANA KAMA UPENDO

## Mtazamo wa Vijana

KING'S College LONDON

TAMASHA

YOUNG MAYOR FOR LEWISHAM